



Maswali na Majibu

1. Mbona Daudi alishangaa alipoona hakuna Mwisraeli aliyejitolea kupigana na Goliathi?
Alikuwa na imani kwamba Mungu angewasaida kushinda Goliathi.
2. Daudi aliuuwa Goliathi namna gani?
Jiwe kwa kombeo. Halafu akakata kichwa chake.
3. Mbona Sauli alikuwa na wivu kwa Daudi.
Mungu alikuwa amemkataa na alijua Daudi ndiye atakuwa mfalme baada ya yeye.
4. Nani alikuwa rafiki mkuu wa Daudi? Daudi alimwaahidi nini?
Yonathani, mwana wa Sauli. Atakapokuwa mfalme atakuwa mzuri kwa familia ya Yonathani.
5. Daudi aliishi wapi alipokuwa akitoroka kutoka kwa Sauli?
Aliishi kwa vilima, mwituni na kwa mapango.
6. Daudi alifanya nini Sauli alipokuja kwa pango alilokuwa amejificha?
Daudi alikata kipande kwa joho ya Sauli kuonyesha alikuwa na nafasi ya kumuua.
7. Daudi alifanya nini alipopata Sauli analala?
Daudi alichukua mkuki na birika ya maji ya Sauli.
8. Mbona Daudi hakuua Sauli wakati alipata nafasi ya kumuua.
Kwa sababu Sauli alikuwa mfalme, mpakwa mafuta wa Mungu.
9. Nini ilifanyika kwa Mlima wa Gilboa?
Sauli na wana wake 3 waliuawa.
10. Daudi alitimiza ahadi gani kwa Yonathani?
Alikuwa mzuri kwa familia ya Yonathani.

Mistari ya kukariri

1 Samweli 17:45 1 Samweli 26:23 – 24 2 Samweli 1:23, 26 na 27

Mazungumzo

Mungu alikuwa anaandaa Daudi kuwa mfalme. Zungumzia matendo yenye Daudi alifanya kwa hili somo. Daudi alichukuaje wakati Goliathi alidharau Waisraeli? Alikuwa kiongozi wa namna gani? Alichukuaje wakati alikuwa na nafasi ya kumuua Sauli? Alichukuaje wakati alisikia kwamba Sauli amekufa. Haya yote yalimsaidia namna gani kuwa mfalme mzuri?

Kuandika

Andika vile Daudi aliuuwa Goliathi.

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

Somo la 21 Daudi – mtu wa Mungu

SOMA 1 Samweli 17:40 – 51; 24:2 – 12; 26:7 -17;

SOMO

Sauli alikuwa mfalme wa kwanza wa Waisraeli. Alianza kuwa na maringo na kuasi Mungu. Mungu alimkataa kuwa mfalme. Mungu alikuwa amemchagua Daudi kuwa mfalme baada yake.

Ndugu wa Daudi walikuwa kwa jeshi la Sauli. Walikuwa wakipigana na maadui wao, Wafilisti. Siku moja Daudi alienda kuapelekeea ndugu zake chakula. Waisraeli walipiga kambi upande moja wa bonde na Wafilisti nao walipiga kambi upande mwingine. Jitu mkubwa aitwae Goliathi aliwapa Waisraeli changa moto. Aliwambia Waisraeli wachague mtu mmoja apigane naye. Lakini Waisraeli wote waliogopa.

Goliathi alikuwa anadharau watu wa Mungu. Daudi alishangaa alipoona hukuna Mwisraeli hata mmoja aliyekuwa shujaa na ajitokeze kupigana naye. Alijua Mungu atasaidia watu wake kuwapiga maadui wao.

Daudi alisema kwamba atapigana na Goliathi. Sauli alisema eti Daudi ni mtoto tena hajajifunza kupigana. Lakini Daudi aliambia Sauli kwamba Mungu atamsadia. Mungu alikuwa amemsaidia kuua simba na dubu waliotaka kuua kondoo wake. Mungu atamsaidia amuue jitu, Goliathi aliyekuwa anadharau jeshi la Mungu. Sauli alikubali.

Daudi alienda kupigana na Goliathi akiwa na fimbo ya mchungaji na kombeo. Alichagua vijiwe vyta mviringo kutoka kwa mto. Goliathi aliudhika sana alipoona kijana ndiye anakuja kupigana na yeye. Alitarajia mtu wa nguvu kutoka kwa jeshi ajitokeze ili wapigane. Alipaza sauti na kusema, "Mimi ni mbwa hata unanijia kwa fimbo na mawe." Daudi alimjibu, Wewe unanijia kwa upanga, fumo, na mkuki na mimi ninakujia wewe kwa jina la Bwana wa majeshi, Mungu wa majeshi ya Israeli." Goliathi alipokuwa akikimbia kumkujia, Daudi aliweka jiwe kwa kombeo yake na kutupa. Jiwe lilimpiga Goliathi kwa kipaji na Goliathi akaanguka kifudifudi na kufa. Daudi alikata kichwa chake. Wafilisti wote walitoroka huku wakifukuzwa na Waisraeli.

Sauli alikuwa na wivu kwa Daudi. Sauli alijua kwamba Daudi ndiye atakuwa mfalme baada ya yeye. Aliona vile Mungu alimsaidia kwa vita. Sauli aliona wivu na kuhuzunika sana. Daudi alikuja kumchezea kinubi ili achangamke. Siku moja Sauli alitupia Daudi mkuki alipokuwa akimchezea kinubi ili amuue. Daudi aliheba na kutoroka.

Yonathani alikuwa mwana wa Sauli. Alikuwa rafiki mkuu wa Daudi. Yonathani alijua kwamba Daudi ndiye atakuwa mfalme badala yake lakini hakuwa na wivu. Alijua ni mapenzi ya Mungu. Yonathani alisaidia Daudi. Wote wawili walifanya agano kuu katikati yao. Waliahidiana kwamba watacaa kama marafiki wazuri. Yonathani aliahidi Daudi kwamba atamsaidia asiuawe. Daudi aliahidi kwamba atakopokuwa mfalme, atalinda Yonathani pamoja na familia yake.

Daudi aliogopa kwenda nyumbani. Yonathani akamwabia kwamba atachunguza kuona kama Sauli bado ana hasira kwa Daudi. Kweli Sauli alikuwa bado anataka kumuua Daudi. Kwa hivyo Yonathani alisaidia Daudi kutoroka.

Ilibidi Daudi ajiponye maisha yake. Alikuwa mtoro kwa miaka fulani. Alijificha kwa vilima, mwituni na kuishi kwa mapango. Sauli alituma wapelelezi wake kutafuta Daudi ili amuue.

Daudi alikuwa na wafwasi wake kwa huo muda aliokuwa mtoro. Daudi alikuwa kiongozi mzuri kwa sababu alifunza watu wake kupenda Mungu na kutii amri. Wakati wote walikuwa wakimchunguza Sauli alikokuwa pamoja na watu wake. Walichificha kwa mwiamba na mapango ndani ya vilima. Sauli aliendelea kutafuta Daudi ili amuue.



Wapelelezi wa Sauli walikundua kwamba Daudi alikuwa amejificha kwenye jangwa la Engendi. Sauli na jeshi lake walienda kutafuta Daudi ili wamuue. Daudi na watu wake waliishi kwa pango lililokuwa na kina kirefu sana. Walipoona Sauli na jeshi lake wanakuja, walisongea ndani kwa giza kabisa ndani ya hilo pango.

Sauli alienda ndani ya hilo pango kupumzika. Watu wa Daudi walimwambia huo ulikuwa wakati wa kuua Sauli na kulibisha kisasi. Lakini Daudi hangeua Sauli kwa sababu Sauli alikuwa mfalme Masihi wa Mungu.

Daudi aliamini Mungu. Alijua Mungu atamfanya mfalme wakati utakapotimia. Alijua Mungu atatimiza ahadi Yake kwa kumfanya awe mfalme baadaye.

Daudi alikata kipande cha joho ya Sauli kuonyesha alikuwa na nafasi ya kumuua. Sauli alipotoka inje ya pango, Daudi alimwitia na akamwonyesha kipande cha joho alichokata. Daudi alimwambia kwamba alikuwa na nafasi ya kumuua, lakini hakutaka.

Sauli alipoona kwamba Daudi hakutaka kumuua, aliahidi Daudi kwamba hatarajibu kumfuata tena na amuue. Sauli na jeshi lake walirudi nyumbani na kwa muda Daudi na watu wake wakawa salama.

Lakini ilikuwa kwa muda mfupi na Sauli alibadilisha mawazo na akawa na wivu tena. Alienda na jeshi lake kumtafuta Daudi. Usiku moja Daudi alienda polepole mpaka kwa kambi ya Sauli. Sauli na watu wake walikuwa wamelala fo fo fo. Mtu wa Daudi alimwambia amuua Sauli. Lakini Daudi hakumuua Sauli kwa sababu Sauli ni mfame, Masihi wa Mungu. Wakati huu Daudi alichukuwa mkuki na birika ya maji ya Sauli kuonyesha kwamba alikuwa na nafasi ya kumuua tena. Mara tena, Sauli alijua kwamba Daudi alikuwa na nafasi ya kumuua na akaahidi hatamuua tena.



Wafilisti walikuja kupigana na Waisraeli tena. Hivi vita vilikuwa kwa Mlima wa Gilboa. Sauli na Waisraeli walikuwa wamemwacha Mungu, kwa hivyo Mungu hakuwa akiwasaidia. Wafilisti walishinda Waisraeli. Waisraeli walitoroka na wengi waliuawa. Sauli na wanawe watatu walikufa pamoja na Yonathani. Daudi aliposikia kwamba Sauli na Yonathani wamekufa, alilia sana. Daudi alitimiza ahadi yake kwa Yonathani na akawa mzuri kwa familia ya Yonathani.

Daudi alikuwa sasa mfalme. Alipenda Mungu na akasaidia watu kuabudu na kumtii Mungu. Daudi alikuwa na uwezo wote lakini alikumbuka kumpenda na kumtii Mungu. Alikuwa mfalme wa nguvu.

Daudi alikuwa mtu wa Mungu. Alipenda na kumwamini Mungu. Wakati alimpiga Goliathi aliamini kwamba Mungu atamsaidia. Alikuwa na imani kwamba hawezo kumuua Sauli mfalme, masihi wa Mungu. Alijua yeye ndiye atakuwa mfalme baada ya Sauli kwa wakati wa Mungu ufaao. Alitimiza ahadi yake kwa Yonathani. Alikuwa na imani kuu kwa Mungu.